Masomo: Sera ya SHS Financial Assistance (Charity Care)	**Nambari ya Hati ya Bima:** PSJH RCM 0002 SHS	
Idara: Revenue Cycle Management	☒ Mpya ☐ Ilikaguliwa ☐ Imepitiwa	**Tarehe:** 3/22/2019
Mfadhili Mkuu: Kimberly Sullivan, SVP Chief Revenue Cycle Officer	**Mmiliki wa Hati ya Bima:** Lesa Ellis, Mkurugenzi wa Ushauri wa Fedha na Usaidizi	
Imeidhinishwa na: Halmashauri ya Wakurugenzi ya PSJH	**Tarehe ya Utekelezaji:** 5/1/2019	

Swedish Health Services na Swedish Edmonds (“SHS” au “Swedish”) ni shirika la afya lisilo la faida linaloongozwa kwa ahadi ya Lengo lake la kuboresha afya na hali njema ya kila mtu tunayemhudumia, kwa Maadili yake Msingi ya usalama, huduma inayolenga mgonjwa, heshima, kujali na mapenzi, ushirikiano na ubia, kuendelea kujifunza na kuboresha na uongozi na kwa imani kuwa huduma ya afya ni haki ya binadamu. Ni falsafa na desturi ya kila hospitali ya SHS kuwa huduma za dharura na zinazohitajika za afya zipatikane kwa wale walio katika jamii tunazohudumia, bila kujali uwezo wao wa kulipa.

WIGO

Sera hii inatumika kwenye hospitali zote za SHS na kwa huduma zote za dharura na za haraka na zinazohitajika za afya zinazotolewa na hospitali za SHS (bila kujumuisha huduma ya majaribio au uchunguzi). Orodha ya hospitali za SHS zinazoshughulikiwa na sera hii inaweza kupatikana katika Exhibit A Covered Facilities List.

Sera hii itafasiriwa kwa njia inayolingana na Sehemu ya 501(r) ya Internal Revenue Code ya 1986, kama ilivyorekebishwa. Endapo kutatokea mgogoro kati ya vipengee vya sheria kama hizo na sera hii, sheria hizo zitatawala.

MADHUMUNI:

Madhumuni ya sera hii ni kuhakikisha mbinu ya usawa, isiyo ya ubaguzi na inayofanya kazi kwa kipengee cha Usaidizi wa Fedha (huduma ya msaada) kwa watu wanaostahiki ambao hawawezi kulipia huduma zote za dharura zinazohitajika kimatibabu na nyingine za hospitali zinazotolewa na hospitali za SHS.

Ni nia ya sera hii kuzingatia sheria zote za shirikisho, jimbo na serikali za mtaa. Sera hii na mipango ya usaidizi wa fedha iliyo hapa ina Sera ya Usaidizi wa Fedha (‘FAP’) na Sera ya Huduma ya Matibabu ya Dharura kwa kila hospitali inayomilikiwa, kukodishwa au kuendeshwa na SHS.

SERA:

SHS itatoa huduma za hospitali bila malipo au gharama zilizopunguzwa kwa wagonjwa wanaostahiki wenye mapato ya chini, wasio na bima na walio na bima ya chini wakati uwezo wa kulipia huduma ni kikwazo cha kupata huduma ya dharura inayohitajika kimatibabu na nyingine ya hospitali na hakuna chanzo mbadala cha bima kimetambuliwa. Lazima wagonjwa watimize mahitaji ya kustahiki yaliyoelezwa katika sera hii ili kuhitimu.

Hospitali za SHS zenye idara za dharura zitatoa huduma ya hali za matibabu za dharura bila ubaguzi (ndani ya maana ya Sheria ya Matibabu ya Dharura na Leba) kulingana na uwezo ulipo bila kujali ikiwa mtu anastahiki kwa usaidizi wa fedha. SHS haitabagua kwa msingi wa umri, mbari, rangi, imani, kabila, dini, asili ya taifa, hadhi ya ndoa, jinsia, mvuto wa jinsia, utambulisho au mwelekeo wa jinsia, ulemavu, hali ya ukongwe au jeshi, au msingi mwingine wowote uliopigwa marufuku na sheria ya shirikisho, jimbo au serikali za mtaa wakati wa kufanya maamuzi ya usaidizi wa fedha.

Hospitali za SHS zitatoa huduma za dharura za chunguzi za matibabu na tiba ya uimarishaji, au kutoa rufaa na uhamisho wa mtu ikiwa uhamisho huo unafaa kwa mujibu wa 42 C.F.R 482.55. SHS inapiga marufuku vitendo vyovyote, desturi za kulaza, au sera ambazo zinaweza kuwavunja moyo watu wanaohitaji huduma ya matibabu ya dharura, kama vile kuruhusu shughuli za ukusanyaji wa madeni zinazohitilafiana na utoaji wa huduma ya matibabu ya dharura.

Orodha ya Watoa Huduma Kulingana na SHS FAP: Kila hospitali ya SHS itatambua orodha ya madaktari, vikundi vya matibabu, au wataalamu wengine wanaotoa huduma ambao wanafidiwa au hawafidiwi na sera hii. Kila hospitali ya SHS itatoa orodha hii kwa mgonjwa yeyote anayeomba nakala. Orodha ya watoa huduma pia inaweza kupatikana mtandaoni kwenye tovuti ya SHS: www.swedish.org.

Mahitaji ya Ustahiki wa Usaidizi wa Fedha: Usaidizi wa fedha unapatikana kwa wagonjwa wenye bima na wasio na bima na wadhamini ambapo usaidizi kama huo unalingana na sera hii na sheria za shirikisho na jimbo zinazoongoza manufaa yanayoruhusiwa kwa wagonjwa. Hospitali za SHS zitafanya jitihada zinazofaa ili kuamua uwepo au kutokuwepo kwa bima nyingine inayoweza kupatikana, kwa jumla au kiasi, kwa huduma inayotolewa na hospitali za SHS, kabla ya kuelekeza jitihada zozote za ukusanyaji kwa mgonjwa.

Wagonjwa wanaotafuta usaidizi lazima wakamilishe Ombi la kawaida la Usaidizi wa Fedha la SHS na ustahiki utalingana na hitaji la fedha kuanzia tarehe ya huduma au tarehe ya ombi, inavyotumika. Wagonjwa wanaweza kutuma ombi jingine la usaidizi ikiwa hali zao za fedha zitakuwa mbaya zaidi baada ya muda, hata ikiwa ombi la awali lilikataliwa au kuidhinishwa kiasi. Jitihadi zinazofaa zitafanywa ili kuwaarifu na kuwafahamisha wagonjwa kuhusu upatikanaji wa Usaidizi wa Fedha kwa kutoa taarifa wakati wa kulazwa na kuruhusiwa kutoka, mawasiliano ya maandishi kuhusu bili au ukusanyaji, bili ya huduma ya mgonjwa wa kulazwa au sehemu ya huduma za fedha, kwenye tovuti ya hospitali ya SHS, kwa arifa ya mdomo wakati wa majadiliano ya malipo na pia ishara katika maeneo yenye idadi ya juu ya wagonjwa wa kulazwa na wasio wa kulazwa, kama vile idara ya kulaza na dharura. Tafsiri zitapatikana kwa lugha yoyote inayozungumzwa na zaidi ya asilimia kumi ya idadi katika eneo la huduma ya hospitali.

Kutuma Ombi la Usaidizi wa Fedha: Wagonjwa au wadhamini wanaweza kuomba na kuwasilisha Ombi la Usaidizi wa Fedha, ambalo ni la bila malipo na linaptikana kwenye wizara ya SHS au kwa njia zifuatazo: kushauri wafanyakazi wa huduma za fedha kwa wagonjwa wakati wa au kabla ya wakati wa kuruhusiwa kutoka kuwa usaidizi unaombwa na kuwasilishwa kwa nyaraka zilizokamilishwa; kwa barua pepe, au kwa kutembelea www.swedish.org, kupakua na kuwasilisha ombi la nyaraka zilizokamilishwa. Mtu anayetuma ombi la usaidizi wa fedha atafanyiwa uchunguzi wa mwanzo, utakaojumuisha ukaguzi wa ikiwa mgonjwa ametumia au hastahiki kwa vyanzo vyovyote vya malipo mengine.

Kila hospitali ya SHS itakuwa na mfanyakazi aliyeteuliwa kuwasaidia wagonjwa wanaokamilisha Ombi la Usaidizi wa Fedha na kuamua ustahiki kwa ajili ya usaidizi wa fedha wa SHS au usaidizi wa fedha kutoka kwenye mipango ya bima inayofadhiliwa na serikali ikiwa ipo. Huduma za ukalimani zinapatikana ili kushughulikia swali au suala lolote na kusaidia kukamilisha Ombi la Usaidizi wa Fedha.

Mgonjwa au mdhamini anayeweza kustahiki kutuma ombi la usaidizi wa fedha anaweza kuipa SHS nyaraka za kutosha ili kuthibitisha uamuzi wa ustahiki wakati wowote baada ya kujua kuwa mapato ya mhusika yako chini ya FPL kwa mujibu wa sheria husika za Shirikisho na Jimbo.

SHS inakiri kuwa kwa mujibu wa Washington Administrative Code (WAC) 246-453-020, uamuzi wa ustahiki unaweza kufanywa wakati wowote baada ya kufahamu kuwa mapato ya mhusika ni chini ya 200% ya wastani wa umaskini wa shirikisho. Mbali na hayo, SHS inaweza uamua kutoa usaidizi wa fedha kulingana na uamuzi wa mwanzo wa hali ya mgonjwa kama mtu maskini, kama ilivyofafanuliwa katika WAC 246-453-010. Katika hali hizi, huenda nyaraka zisihitajike.

Hali ya Fedha ya Mtu Binafsi: Mapato, rasilimali za pesa na gharama za mgonjwa zitatumiwa kutathmini hali ya fedha ya mgonjwa. Kwa madhumuni ya FAP, Washington inafafanua mapato na familia kulingana na WAC 246-453-010. Rasilimali za pesa hazitajumuisha kustaafu wala mipango ya fidia iliyoahirishwa inayohitimu chini ya Interna Revenue Code wala mipango ya fidia iliyoahirishwa isiyo ya kuhitimu. Rasilimali za pesa hazitatumiwa kwa uamuzi wa ustahiki ikiwa mapato ya mgonjwa au mdhamini ni au chini ya 200% ya kiwango cha umaskini wa shirikisho.

Uhitimu wa Mapato: Vigezo vya mapato kulingana na Kiwango cha Umaskini cha Jimbo (FPL), vinaweza kutumiwa kuamua ustahiki wa huduma bila malipo wala huduma ynye punguzo. Tafadhali tazama Exhibit B kwa maelezo.

Maamuzi na Idhini: Wagonjwa watapokea arifa ya uamuzi wa ustahiki wa FAP ndani ya siku 14 za wasilisho la ombi lililokamilishwa la Usaidizi wa Fedha na nyaraka muhimu. Pindi tu ombi linapopokelewa, jitihada za kipekee za ukusanyaji zitawekwa hadi uamuzi wa maandishi wa ustahiki utumwe kwa mgonjwa. Hospitali haitafanya uamuzi wa ustahiki kwa ajili ya usaidizi kulingana na taarifa ambayo hospitali inaamini si sahihi wala ya kuaminika.

Suluhisho la Mgogoro: Mgonjwa anaweza kukata rufaa ya uamuzi wa kutostahiki kwa usaidizi wa fedha kwa kutoa nyaraka muhimu za ziada kwa hospitali ndani ya siku 30 baada ya kupokea ilani ya kukataliwa. Rufaa zote zinakaguliwa na ikiwa ukaguzi utathibitisha kukataliwa, arifa ya maandishi itatumwa kwa mdhamini na Idara ya Afya ya Jimbo, ambapo inahitajika na kwa mujibu wa sheria. Mchakato wa mwisho wa rufaa utahitimishwa ndani ya siku 10 baada ya kupokea ukataliwaji na hospitali. Rufaa inaweza kutumwa Swedish Medical Center, Wito: Corporate Business Office, 747 Broadway, Seattle, WA 98122.

Msaada wa Kutarajiwa: SHS inaweza kuidhinisha mgonjwa kwa ajili ya marekebisho ya msaada kwenye salio la akaunti yake kwa njia ambayo si ombi kamili la Usaidizi wa Fedha. Maamuzi kama hayo yatafanywa kwa msingi wa kutarajiwa kwa kutumia zana ya tathmini ya fedha inayotambuliwa na tasnia ambayo inatathmini uwezo wa kulipa kulingana na rekodi za fedha zinazopatikana kwa umma au rekodi nyingine, ikiwemo lakini si tu mpato ya familia, ukubwa wa familia na historia ya mikopo na malipo.

Hali Nyingine za Kipekee: Wagonjwa wanaostahiki mipango ya kuhitimu ya FPL kama vile Medicaid na mipango mingine ya usaidizi wa mapato ya chini inayofadhiliwa na serikali, wanasemekama kuwa maskini. Kwa hivyo, wagonjwa kama hao wanastahiki Usaidizi wa Fedha wakati mipango inawanyima malipo na kisha kuona kuwa ada zinatozwa mgonjwa. Masalio ya akaunti ya mgonjwa yanayotokana na ada ambazo hazikufidiwa yanastahiki kufutiliwa mbali kikamilifu kwa msaada. Illiyojumuishwa mahususi kama inayostahiki ni ada zinazohusiana na yafuatayo:

- Mgonjwa kunyimwa uwezo kuendelea kukaa
- Siku za huduma ambazo mgonjwa alinyimwa
- Huduma zisizofidiwa
- Kunyimwa Idhini Kabla ya Matibabu
- Kunyimwa kutokana na bima yenye vikwazo

Gharama za Ajabu za Matibabu: SHS, kwa busara yake, inaweza kutoa msaada endapo kuna gharama ya ajabu ya matibabu. Wagonjwa hawa watashughulikiwa kwa msingi wa mtu binafsi.

Vikwazo kwenye Ada za Wagonjwa wote Wanaostahiki Usaidizi wa Fedha: Hakuna mgonjwa anayehitimu kwa yoyote ya kategoria zilizo hapo juu za usaidizi atawajibika binafsi kwa zaidi ya asilimia ya “Amounts Generally Billed” (AGB) ya ada za jumla kama ilivyofafanuliwa.

Mpango wa Malipo Unaofaa: Pindi tu mgonjwa anapoidhinishwa kwa usaidizi kiasi wa fedha, lakini bado ana salio linalohitaji kulipwa, SHS itajadili mpango wa malipo. Mpango wa malipo unaofaa utakuwa na malipo ya kila mwezi ambayo si zaidi ya asilimia 10 ya mapato ya mgonjwa au familia ya kila mwezi, isipokuwa makato ya Essential Living Exppenses ambayo mgonjwa ameorodhesha kwenye ombi lake la usaidizi wa fedha.

Bili na Ukusanyaji: Masalio yoyote ambayo hayajalipwa ambayo wagonjwa au wadhamini wanadaiwa baada ya ombi la mapunguzo yaliyopo, ikiwa yapo, yanaweza kuwekwa kwenye ukusanyaji. Jitihada za ukusanyaji kuhusu masalio ambayo hayajalipwa zitakoma zikisubiri uamuzi wa ustahiki wa FAP. SHS haitekelezi, kuruhusu wala kuruhusu mashirika ya ukusanyaji kutekeleza hatua zozote za ukusanyaji wa kipekee kabla ya: (a) kufanya jitihada inayofaa ili kuamua ikiwa mgonjwa anahitimu kwa usaidizi wa fedha; au (b) siku 120 baada ya taarifa ya kwanza ya mgonjwa kutumwa. Kwa taarifa kuhusu bili ya SHS na desturi za ukusanyaji kwa pesa ambazo wagonjwa wanadaiwa, tafadhali tazama sera ya Hospitali ya SHS, ambayo inapatikana bila malipo kwenye kila meza ya usajili ya hospitali ya SHS, au kwenye: www.swedish.org**.**

Fedha Zinazorejeshewa Mgonjwa: Endapo mgonjwa au mdhamini amelipia huduma na baadaye kuamuliwa kustahiki kwa huduma ya bila malipo au yenye punguzo, malipo yoyote yaliyotolewa yanayohusiana na huduma hizo wakati wa kustahiki kwa FAP unaozidi jukumu la malipo yatarejeshwa, kwa mujibu wa sheria za jimbo.

Ukaguzi wa Kila Mwaka: Sera hii ya Providence Financial Assistance (Charity Care) itakaguliwa kila mwaka na uongozi teule wa Revenue Cycle.

VIGHAIRI:
Tazama Wigo hapo juu.

UFAFANUZI:
Kwa madhumuni ya sera hii ufafanuzi na mahitaji yafuatayo yanatumika:

1. Kiwango cha Umaskini cha Shirikisho (FPL): FPL inamaanisha miongozo ya umaskini inayosasishwa kila mara katika Sajili ya Shirikisho na Idara ya Afya na Huduma ya Binadamu ya Marekani.

2. Pesa Zinazotozwa kwa Jumla (Amounts Generally Billed, AGB): Pesa zinazotozwa kwa jumla kwa ajili ya dharura na huduma nyingine muhimu ya matibabu kwa wagonjwa walio na bima ya afya zinajulikana katika sera hii kama AGB. SHS inaamua asilimia ya AGB inayotumika kwa kuzidisha ada za jumla za hospitali kwa huduma yoyote muhimu ya dharura au matibabu kwa asilimia isiyobadilika kulingana na madai yanayoruhusiwa chini ya Medicare. Karatasi za taarifa zilizo na maelezo ya asilimia za AGB na jinsi zinavyokokotolewa, zinaweza kupatikana kwa kuenda kwenye tovuti ifuatayo: www.swedish.org au kwa kupiga simu **1-866-747-2455** au kuomba nakala.

3. Hatua ya Ukusanyaji ya Kipekee (Extraordinary Collection Action, ECA): ECA zinafafanuliwa kama hatua zinazohitaji mchakato wa kisheria au mahakama, zinahusu kuuza deni kwa mtu mwingine au kuripoti taarifa mbaya kwenye mashirika ya mikopo au rasimu. Hatua zinazohitaji mchakato wa kisheria au mahakama kwa madhumuni haya zinajumuisha; utwaaji wa mali halisi; ukamataji au ufungaji wa akaunti ya benki au mali mengine ya binafsi; uanzishaji wa hatua ya raia dhidi ya mtu binafsi; hatua zinazosababisha kukamatwa kwa mtu binafsi; hatua zinazosababisha mtu binafsi kukamatwa kwa agizo la mahakama; na kuzuiwa kwa ujira kwa ajili ya madeni kwa agizo la mahakama.

MAREJEO:

Internal Revenue Code Sehemu ya 501(r); 26 C.F.R. 1.501(r)(1) – 1.501(r)(7)
Washington Administrative Code (WAC) Sura ya 246-453
Revised Code of Washington (RCW) Sura ya 70.170.060
Sheria ya Emergency Medical Treatment and Labor (EMTALA), 42 U.S.C. 1395dd
42 C.F.R. 482.55 na 413.89
Miongozo ya American Hospital Associations Charity
Providence St. Joseph Health Commitment kwa Miongozo ya Wasio na Bima
Provider Reimbursement Manual, Sehemu ya I, Sura ya 3, Sehemu ya 312

Kizibiti A – Orodha ya Vituo vyenye Bima

Hospitali za SHS huko Washington	
Swedish Medical Center First Hill/Ballard	Swedish Medical Center Cherry Hill
Swedish Issaquah	Swedish Edmonds

Kizibiti B - Kuhitimu kwa Mapato kwa hospitali za SHS

Wakati wa Maamuzi ya Mapato: Mapato ya familia ya kila mwaka ya mgonjwa yataamuliwa kuanzia wakati huduma za hospitali zilitolewa, au wakati wa ombi ikiwa ombi limefanywa ndani ya miaka miwili ya wakati huduma zilitolewa na mgonjwa amekuwa akifanya jitihada njema za malipo ya huduma.

Ikiwa...	Basi ...
Mapato ya familia ya kila mwaka, yakirekebishwa kwa ukubwa wa familia, ni au chini ya 300% ya miongozo ya sasa ya FPL,	Mgonjwa anaamuliwa kuwa maskini kifedha na kuhitimu kwa usaidizi wa fedha kwa kuondolewa 100% kwenye pesa za jukumu la mgonjwa.[1]
Mapato ya familia ya kila mwaka, yakirekebishwa kwa ukubwa wa familia, ni kati ya 301% na 400% ya miongozo ya sasa ya FPL,	Mgonjwa anastahiki punguzo la 75% kutoka ada za asili kwenye pesa za jukumu la mgonjwa.
Ikiwa mapato ya familia ya kila mwaka, yakirekebishwa kwa ukubwa wa familia ni au chini ya 400% FPL NA mgonjwa amepata gharama za jumla za matibabu kwenye hospitali za SHS kabla ya miezi 12 zaidi ya 20% ya mapato yao ya familia ya kila mwaka, yakirekebishwa kwa ukubwa wa familia, kwa huduma zinazolingana na ukubwa huu.	Mgonjwa anastahiki manufaa ya msaada wa 100% kutoka kwenye pesa za jukumu la mgonjwa.

[1] kulingana na WAC Ch. 246-453, mradi tu watu kama hao hawastahiki kwa ufadhili mwingine (tazama RCW 70.170.020(5) na 70.170.060(5)).